THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

FASIHI YA KISWAHILI
School Based Assessment
Gredi ya 10
2026
Kazimradi

MWONGOZO WA KUTATHMINIA

Maelekezo kwa Mwalimu

1. *Kazimradi hii ina mazoezi yanayomwezesha mwanafunzi kudhihirisha uelewa wa nyimbo na fasihi simulizi kwa jumla.*
2. *Waelekeze wanafunzi kutekeleza shughuli zote katika kazimradi hii.*
3. *Waelekeze wanafunzi kuhakikisha wameshiriki kikamilifu katika kila zoezi. Hivyo, wape wanafunzi muda mwafaka wa kujiandaa na kutekeleza shughuli zote.*
4. *Tathmini mazoezi yote kwa kurejelea vigezo na viwango vya utuzaji vilivyo katika mwongozo huu wa kutathminia.*
5. *Umilisi wa kimsingi na maadili yamefumbatwa kwenye mazoezi yote.*
6. *Tathmini umilisi wa kimsingi na maadili mwanafunzi anaposhughulikia kazimradi.*
7. *Tumia orodha hakiki iliyo katika mwongozo huu kutathmini umilisi wa kimsingi unaolengwa kukuzwa.*
8. *Wape wanafunzi maoni ya mara kwa mara ili kuwawezesha kuboresha kazi zao na kufanikisha shughuli zote tarajiwa. Yawe maoni ya kuhimiza utendakazi.*
9. *Waelekeze wanafunzi kuweka rekodi ya kazi zao kwenye potifolio.*
10. *Mazoezi yote yafanywe na alama kuwasilishwa kabla ya tarehe 31/10/2026.*

Mwongozo huu una kurasa 12 zilizopigwa chapa.

© 2026 The Kenya National Examinations Council

Vigezo vya kutathminia (alama 60)

Zoezi	Kigezo	Alama
Zoezi la 1	Kufanya utafiti kuhusu moja kati ya aina za nyimbo katika jamii	10
Zoezi la 2	Kufanya uchanganuzi wa wimbo uliofanyiwa utafiti	15
Zoezi la 3	Kuwasilisha wimbo uliofanyiwa utafiti	20
Zoezi la 4	Kuandika ripoti ya utafiti uliofanywa	15

1. **Zoezi la 1: Kufanya utafiti kuhusu moja kati ya aina za nyimbo katika jamii**

a) Mwanafunzi ateue angalau aina moja ya wimbo kutoka kwa orodha aliyopewa.

b) Mwanafunzi afanye utafiti kuhusu wimbo aliouteua kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:

i. Aina ya wimbo

ii. Waliouimba wimbo huo

iii. Walioimbiwa wimbo huo

iv. Sababu za kuuimba wimbo huo

v. Wakati wimbo huo ulipoimbwa

vi. Mahali wimbo huo ulikoimbiwa

vii. Utamaduni unaohusishwa na wimbo huo

viii. Historia inayohusishwa na wimbo huo

(hoja 8x1=8)

c) Hakiki wimbo ulioandikwa na mwanafunzi kwa lugha asilia na tafsiri yake. (alama 2)

Tanbihi

Waelekeze wanafunzi katika shughuli zilizopendekezwa kwenye sehemu ya d,e,f na g.

2. **Zoezi la 2: Kufanya uchanganuzi wa wimbo uliofanyiwa utafiti**

a) Uchanganuzi wa vipengele vifuatavyo katika wimbo ambao mwanafunzi aliufanyia utafiti ubainishwe.

i. Ujumbe/maudhui/maadili

ii. Sifa

iii. Umuhimu wa wimbo huo katika jamii

iv. Mitindo ambayo jamii ilitumia kuwasilisha aina ya wimbo alioutafitia.

Zifuatazo ni baadhi ya hoja katika kila kipengele.

i. Ujumbe/Maudhui katika nyimbo

Kwa mfano:

- Maadili
- Elimu
- Malezi
- Utamaduni
- Uwajibikaji

- Mapenzi/upendo
- Mshikamano wa kijamii
- Imani na dini
- Maombolezi

(Hoja 4x1)

ii. Sifa za Nyimbo

- Nyimbo hutolewa kwa mahadhi ya kupanda na kushuka kwa sauti.
- Hutumia lugha ya mkato yenye mpangilio maalum wa silabi, mishororo na beti zenye mapigo ya kimuziki.
- Hutumia lugha nzito yenye kuibua taswira na hisia nzito kama za mapenzi, huzuni au furaha.
- Zinapoimbwa, mara nyingi huandamana na ala za muziki kama vile ngoma, baragumu na zumari.
- Katika jamii za kiafrika, nyimbo hufungamana na muktadha fulani. Kuna nyimbo za kazi, harusi, jando na unyago au hata kumpa mtoto jina.
- Baadhi ya vifungu katika nyimbo hurudiwarudiwa. Vifungu hivi huitwa vibwagizo, viitikio au mikarara ya nyimbo.
- Nyimbo nyingi huandamana na uchezaji wa viungo kama vile mabega, kupiga makofi na mapigo ya miguu.
- Kimsingi, nyimbo ziliimbwa na makundi ya watu kwa hadhira hai. Hata hivyo, kuna nyimbo zilizoimbwa na mtu mmoja kwa hadhira yake au hata bila hadhira.

(Hoja 4x1)

iii. Umuhimu wa nyimbo

- Nyimbo hutambulisha jamii kwa kusawiri shughuli na maisha ya jamii iliyozibuni.
- Humwezesha binadamu kutakasa hisia zake.
- Ni mbinu mojawapo ya kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii.
- Nyimbo hutumbuiza/huburudisha.
- Hupitisha amali na mambo ambayo jamii inayathamini.
- Hutumiwa kuhamasisha watu na kuchochea hisia za kuchangamkia jambo fulani.
- Huakisi ukwasi wa tamaduni za jamii.
- Hukuza ubunifu miongoni mwa wanajamii.
- Hutumiwa kuleta mshikamano wa kijamii.

(Hoja 4x1)

iv. Mitindo ambayo jamii ilitumia kuwasilisha aina ya wimbo uliotafitiwa

- Kutumia mtindo wa kupokezana.
- Kutumia lugha inyoibua hisia zifaazo.
- Kuvaa maleba yafaayo.
- Kuambatanisha na upigaji na uchezaji ngoma.
- Kutumia ishara za uso na mwili kulingana na ujumbe unaonuiwa.
- Kubadilisha kiimbo kulingana na ujumbe.
- Kubadilisha kasi kulingana na hisia unazotaka kuibua.

(Hoja 3x1)

Tanbihi

Hakiki majibu ya mwanafunzi ipasavyo.

Waelekeze wanafunzi katika shughuli zilizopendekezwa kwenye sehemu ya b,c,na d.

3. **Zoezi la 3: Uwasilishaji wa wimbo uliofanyiwa utafiti**

Tathmini mawasilisho (uimbaji wa wanafunzi) ukizingatia vigezo vifuatavyo:

a. Sauti
b. Ishara za mwili na uso
c. Mdundo
d. Matamshi
e. Mtiririko wa wimbo
f. Ushirikishwaji wa hadhira
   Tathmini vipengele vitano. (Hoja 5x2=10)

Tanbihi

Waelekeze wanafunzi katika shughuli zilizopendekezwa kwenye swali la a hadi la e.

f) Tumia jedwali lifuatalo kutathmini umilisi wa kimsingi ufuatao:

i. Kujiamini
ii. Mawasiliano na ushirikiano
iii. Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo
iv. Ubunifu

(alama 10)

MWONGOZO WA KUTATHMINIA UMILISI WA KIMSINGI UNAOKUZWA NA MWANAFUNZI

Umilisi wa kimsingi unaotathminiwa	**Maelezo kuhusu umilisi wa kimsingi unaobainika**	**Alama**
Kujiamini	i. Mwasilishaji ana hakika na yale anayoimba. ii. Anasimama kwa mkao ufaao. iii. Anapandisha na kushusha sauti kulingana na hisia anazotaka kuibua. iv. Anadumisha kiwango kifaacho cha sauti. v. Anaipa hadhira nafasi ya kukamilisha mishororo. vi. Anaitazama hadhira ana kwa ana.	3

	vii. Anatamka maneno kwa sauti ifaayo na kwa njia wazi. viii. Anatumia ishara za uso na mwili ipasavyo.	
Mawasiliano na ushirikiano	i. Anatumia lugha nyepesi inayoeleweka kulingana na kiwango cha hadhira. ii. Anatiririsha mawazo kwa kimantiki. iii. Anatamka maneno ipasavyo. iv. Anatumia kasi ifaayo. v. Anabadilisha kiimbo kulingana na hisia anazotaka kuwasilisha. vi. Anawaachia wenzake baadhi ya mishororo wakamilishe. vii. Anatumia ishara na miondoko ipasavyo. viii. Anaimba kwa mdundo ufaao.	3
Ubunifu	i. Anaimba baadhi ya beti kwa mitindo mipya. ii. Anaigiza anapowasilisha baadhi ya mishororo. iii. Anabadilisha kiimbo kulingana na toni anayotaka kuibua.	2
Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo	i. Anaboresha mtindo wa uwasilishaji kulingana na hadhira. ii. Anateua ishara zifaazo kulingana na ujumbe anaotaka kuwasilisha au mazaji anayotaka kuibua.	2

	iii. Anabadilisha baadhi ya maneno ambayo huenda yakatatiza hadhira yake.	

Zoezi la 4: Uandishi wa ripoti

Hakiki ripoti ya mwanafunzi kwa kurejelea jedwali lifuatalo:

Kipengele cha Ripoti	**Kipengele mahususi cha kuzingatia**	**Alama**
Anwani	Mada ya utafiti ibainike: Aina ya wimbo unaotafitiwa ibainike. Kwa mfano: Utafiti wa ujumbe, sifa, dhima na uwasilishaji wa Bembelezi katika jamii ya Wabukusu.	2
Utangulizi	Yafuatayo yadhihirike: Ameonyesha: i. alitafiti kuhusu wimbo upi? ii. alitumia mbinu ipi? iii. alihoji nani (walengwa)? iv. alifanya utafiti wapi?	3
Mwili	Ameonyesha matokeo ya utafiti kama ifuatavyo: Aina ya wimbo aliotafitia: • una historia ipi? • ulikuwa na maudhui na ujumbe upi? • uliimbwa na nani/walengwa • uliimbiwa wapi? • uliimbwa katika muktadha gani wa jamii hiyo? • ulilenga kupititsha ujumbe au maudhui yapi? • ulikuwa na sifa zipi? • kwa nini hasa jamii ikauimba? • uliwasilishwa kwa mitindo ipi?	6
Hitimisho	Amedhihirisha: i. muhtasari wa kazi nzima ii. maoni yake binafsi kuhusu umuhimu wa kazimradi hiyo iii. mchango wa kazimradi hiyo katika kuendeleza ujifunzaji	2
Mapendekezo	Ameonyesha kwa mfano: i. kipengele cha aina hii ya wimbo ambacho hakutafitia ambacho angependa kutafitia baadaye.	2

	ii. aina ya nyimbo za jamii ambazo hakutafitia na kupendekeza utafiti wa baadaye	

Tanbihi

Waelekeze wanafunzi katika kutekeleza shughuli zilizopendekezwa kwenye swali la b, c, d, na e.

VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA

Zoezi la 1 : Kufanya utafiti kuhusu moja kati ya aina za nyimbo katika jamii

Vigezo na Viwango vya kutathminia

Kigezo	**Kuzidi Matarajio** **Kiwango 4**	**Kufikia Matarajio Kiwango 3**	**Kukaribia Matarajio Kiwango 2**	**Chini ya Matarajio Kiwango 1**
Kufanya utafiti kuhusu moja kati ya aina za nyimbo katika jamii	Mwanafunzi anaweza kutambua aina mojawapo ya wimbo na kubainisha waliouimba na walioimbiwa, sababu za kuimbwa,wakati, mahali, utamaduni na historia ya wimbo huo kwa kina.	Mwanafunzi anaweza kutambua aina mojawapo ya wimbo na kubainisha waliouimba na walioimbiwa, sababu za kuimbwa,wakati, mahali, utamaduni na historia ya wimbo huo.	Mwanafunzi anaweza kutambua aina mojawapo ya wimbo na kubainisha waliouimba na walioimbiwa, anatatizika kutambua sababu za kuimbwa,wakati, mahali, utamaduni na historia ya wimbo huo.	Mwanafunzi anaweza kutambua aina mojawapo ya wimbo na kubainisha jina la wimbo, kwa kusaidiwa.
Kuandika wimbo kwa lugha ya asili na kuutafsiri	Mwanafunzi anaandika wimbo kwa lugha ya asili vizuri akizingatia muundo unaofaa na matumizi sahihi ya lugha. Wimbo una ujumbe unaoeleweka bayana. Tafsiri ni sahihi kwa kiwango kikubwa, inahifadhi ujumbe wa wimbo ulivyokuwa katika lugha asilia.	Mwanafunzi anaandika wimbo kwa lugha ya asili akizingatia muundo unaofaa na matumizi sahihi ya lugha. Wimbo una ujumbe unaoeleweka. Tafsiri ni sahihi na inahifadhi ujumbe wa wimbo ulivyokuwa katika lugha asilia.	Mwanafunzi anaweza kuandika wimbo kwa lugha ya asili. Hata hivyo, ana dhihirisha makosa ya kisarufi. Muundo wa wimbo unaonekana kwa kiasi fulani. Tafsiri inaeleweka japo kwa kiwango hafifu. Tafsiri inahifadhi sehemu ya	Mwanafunzi anatatizika katika kuandika wimbo kwa lugha ya asili. Wimbo unakosa muundo wa msingi (beti, kiitikio) lugha ya asili haijatumiwa kwa usahihi. Tafsiri ni dhaifu, ina makosa mengi na haiwasilishi ujumbe wa wimbo ulivyokuwa katika lugha asilia.

Kigezo	Kuzidi Matarajio Kiwango 4	Kufikia Matarajio Kiwango 3	Kukaribia Matarajio Kiwango 2	Chini ya Matarajio Kiwango 1
			ujumbe wa wimbo ulivyokuwa katika lugha asilia.	
Alama	**9-10**	**6-8**	**3-5**	**1-2**

Zoezi la 2: Kufanya uchanganuzi wa wimbo uliofanyiwa utafiti

Kigezo	Kuzidi Matarajio Kiwango 4	Kufikia Matarajio Kiwango 3	Kukaribia Matarajio Kiwango 2	Chini ya Matarajio Kiwango 1
Kubainisha Maudhui katika wimbo	Mwanafunzi anabainisha maudhui manne (4) sahihi yanayopatikana katika wimbo aliouteua. Kila maudhui imefafanuliwa kikamilifu. Ithibati ya maudhui imetolewa kupitia maelezo ya kina yanayotokana na ujumbe katika wimbo.	Mwanafunzi anabainisha maudhui manne (4) sahihi yanayopatikana katika wimbo aliouteua. Kila maudhui imefafanuliwa kikamilifu. Ithibati ya maudhui imetolewa kupitia maelezo yanayotokana na maneno au ujumbe wa wimbo.	Mwanafunzi anabainisha baadhi ya maudhui (mawili au matatu) katika wimbo aliouteua. Maudhui hayo yana uhusiano na wimbo lakini ufafanuzi wake ni wa juu juu. Maudhui yaliyobainishwa yanaelezwa bila mifano kutoka kwenye wimbo.	Mwanafunzi ana changamoto katika kubainisha maudhui katika wimbo aliouteua. Anaweza kutaja wazo moja japo halihusiani moja kwa moja na wimbo. Maudhui hayajafafanuliwa. Ushahidi wa maudhui kutoka kwenye wimbo haupo.
Kueleza sifa za wimbo	Mwanafunzi anabainisha sifa nne (4) za wimbo kwa usahihi na kuzifafanua kwa kina akizingatia vigezo vilivyodokezwa kwenye maagizo. Maelezo yanaonyesha ufahamu mpana wa wimbo. Ufafanuzi unatumia mifano mahususi na lugha ya kuvutia.	Mwanafunzi anabainisha sifa nne (4) za wimbo kwa usahihi na kuzifafanua akizingatia vigezo vilivyodokezwa kwenye maagizo. Maelezo yanaonyesha ufahamu mpana wa wimbo. Ufafanuzi unatumia mifano mahususi.	Mwanafunzi anabainisha baadhi ya sifa za wimbo (sifa mbili au tatu). Sifa hizo zina uhusiano na wimbo, lakini ufafanuzi wake ni wa juu juu. Baadhi ya sifa hazijaelezwa kwa uwazi na mifano haijajitosheleza kikamilifu.	Mwanafunzi anaweza kutaja sifa moja au mbili japo kwa kusaidiwa. Sifa hizo hazijafafanuliwa Maelezo ni dhaifu na hayana ushahidi kutoka kwenye wimbo aliouteua.

Kigezo	Kuzidi Matarajio Kiwango 4	Kufikia Matarajio Kiwango 3	Kukaribia Matarajio Kiwango 2	Chini ya Matarajio Kiwango 1
Kufafanua Umuhimu wa wimbo	Mwanafunzi anafafanua hoja nne (4) kuhusu umuhimu wa wimbo. Hoja alizotoa zimefafanuliwa kikamilifu kwa mifano au maelezo maridhawa.	Mwanafunzi anafafanua hoja nne (4) kuhusu umuhimu wa wimbo. Hoja alizotoa zimefafanuliwa kikamilifu kwa mifano au maelezo kamili.	Mwanafunzi anafafanua baadhi ya hoja (hoja mbili au tatu) kuhusu umuhimu wa wimbo. Hoja alizotoa hazijaelezwa kikamilifu au baadhi yake hazina mifano au maelezo ya kutosha.	Mwanafunzi anaweza kutaja hoja moja au mbili kwa kuelekezwa. Hoja hizo hazina maelezo ya kueleweka au hazihusiani moja kwa moja na wimbo. Ufafanuzi ni dhaifu na hauonyeshi uelewa wa umuhimu wa wimbo katika jamii.
Kueleza mitindo iliyotumiwa na jamii kuwasilisha nyimbo	Mwanafunzi anaeleza kwa ukamilifu na ufasaha mitindo mitatu (3) iliyotumiwa na jamii kuwasilisha nyimbo.	Mwanafunzi anaeleza kwa ukamilifu mitindo mitatu (3) iliyotumiwa na jamii kuwasilisha nyimbo.	Mwanafunzi anaeleza baadhi ya mitindo (mtindo mmoja au mitindo miwili) iliyotumiwa na jamii kuwasilisha nyimbo.	Mwanafunzi anahitaji kuelekezwa ili kutoa maelezo kuhusu mitindo iliyotumiwa na jamii kuwasilisha nyimbo.
Alama	**13-15**	**9-12**	**4-8**	**1-3**

Zoezi la 3: Uwasilishaji wa wimbo uliofanyiwa utafiti

Tumia orodha hakiki ifuatayo kutathmini utendaji wa mwanafunzi katika uimbaji wa wimbo aliouteua.

Tumia viwango vya 1-4 ambapo 4 ina maana ya kuzidisha matarajio, 3 kutimiza matarajio, 2 karibu na matarajio na 1 chini ya matarajio.

Kipengele	Kigezo cha kutathmini	Jinsi ilivyotekelezwa
Sauti	Amepandisha na kushusha sauti ipasavyo.	④ ③ ② ①
Ishara za mwili na uso	Ametumia ishara za mwili na uso ipasavyo.	④ ③ ② ①
Mdundo wa muziki	Amewasilisha kwa sauti yenye mdundo wa kumuziki.	④ ③ ② ①
Hisia	Ametamka maneno yanayoibua hisia zifaazo.	④ ③ ② ①
Mtiririko	Wimbo wake una mtiririko ufaao.	④ ③ ② ①
Hadhira	Ameishirikisha hadhira ipasavyo.	④ ③ ② ①

Zoezi la 4:Uandishi wa ripoti

Kigezo	**Kipengele Mahususi cha Kuzingatia**	**Kuzidisha matarajio**	**Kufikia matarajio**	**Kukaribia matarajio**	**Chini ya matarajio**
Anwani	Mada ya utafiti na aina ya wimbo	Katika uandishi wa mada, mwanafunzi amebainisha kwa ufasaha aina ya wimbo unaotafitiwa, ujumbe, sifa, dhima na uwasilishaji wa wimbo huo.	Katika uandishi wa mada, mwanafunzi amebainisha aina ya wimbo unaotafitiwa, ujumbe, sifa, dhima na uwasilishaji wa wimbo huo.	Katika uandishi wa mada, mwanafunzi amebainisha baadhi ya vipengele, ama aina ya wimbo unaotafitiwa, ujumbe, au sifa, dhima na uwasilishaji wa wimbo huo.	Katika uandishi wa mada, mwanafunzi anahitaji kuelekezwa ili kubainisha aina ya wimbo unaotafitiwa ujumbe, sifa, dhima na uwasilishaji wa wimbo huo.
Utangulizi	Aina ya wimbo, mbinu ya utafiti, walengwa na mahali	Katika utangulizi mwanafunzi amebainisha kwa kina aina ya wimbo, mbinu za utafiti, walengwa na mahali pa utafiti.	Katika utangulizi mwanafunzi amebainisha aina ya wimbo, mbinu za utafiti, walengwa na mahali pa utafiti.	Katika utangulizi mwanafunzi amebainisha baadhi ya vipengele. Ama aina ya wimbo, mbinu za utafiti,au walengwa na mahali pa utafiti.	Mwanafunzi anahitaji kusaidiwa kubainisha aina ya wimbo, mbinu za utafiti, walengwa na mahali pa utafiti.
Mwili	Matokeo ya utafiti (historia, maudhui, walengwa, muktadha, sifa, sababu, mitindo)	Mwanafunzi ametoa ufafanuzi wa kina wa matokeo ya utafiti (historia, maudhui, walengwa, muktadha, sifa, sababu, mitindo).	Mwanafunzi ametoa ufafanuzi wa matokeo ya utafiti (historia, maudhui, walengwa, muktadha, sifa, sababu, mitindo).	Mwanafunzi ametoa ufafanuzi wa sehemu ya matokeo ya utafiti (historia, maudhui, walengwa, muktadha, sifa, sababu, mitindo) japo kwa kiwango hafifu.	Mwanafunzi ametoa ufafanuzi hafifu wa matokeo ya utafiti (historia, maudhui, walengwa, muktadha, sifa, sababu, mitindo) kwa kuelekezwa.
Hitimisho	Muhtasari, maoni binafsi na mchango wa utafiti	Mwanafunzi ametoa muhtasari, maoni binafsi na mchango wa utafiti kwa hoja maridhawa.	Mwanafunzi ametoa muhtasari, maoni binafsi na mchango wa utafiti	Mwanafunzi ametoa muhtasari, maoni binafsi na mchango wa utafiti japo kwa kiwango hafifu.	Mwanafunzi ametoa sehemu ya muhtasari, maoni binafsi na mchango wa utafiti kwa kuelekezwa
Mapendekezo	Mapendekezo ya utafiti wa baadaye	Mwanafunzi ametoa mapendekezo yanayohusiana	Mwanafunzi ametoa mapendekezo yanayohusiana	Mwanafunzi ametoa mapendekezo	Mwanafunzi ametoa baadhi ya mapendekezo.

		moja kwa moja na utafiti wake na yanayoonyesha uelewa mpana.	moja kwa moja na utafiti wake.	yanayohusiana na utafiti wake.	Hata hivyo, baadhi ya mapendekezo hayahusiani na utafiti wake. Anahitaji kuelekezwa.

Mipaka ya kutuzia

Zoezi la 1 (alama 10)

ALAMA	**KIWANGO CHA UTENDAJI**
9-10	4
6-8	3
3-5	2
1-2	1

Zoezi la 2 (alama 15)

ALAMA	**KIWANGO CHA UTENDAJI**
13-15	4
9-12	3
4-8	2
1-3	1

Zoezi la 3 (alama 20)

UPEO/ALAMA	**KIWANGO CHA UTENDAJI**
17-20	4
11-16	3
6-10	2
1-4	1

Zoezi la 4 (alama 15)

UPEO/ALAMA	**KIWANGO CHA UTENDAJI**
13-15	4
9-12	3
4-8	2
1-3	1

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

Assessment score sheet

S/NO	JINA LA MWANAFUNZI	Utafiti kuhusu aina za Nyimbo (alama 10)				Uchanganuzi wa wimbo (alama 15)				Uwasilishaji wa wimbo (alama 20)				Uandishi wa Ripoti (alama 15)				JUMLA
		4	3	2	1	4	3	2	1	4	3	2	1	4	3	2	1	